

Nini huwa kinatokea wakati mtoa huduma wangu wa afya anapochukua kipimo changu?



Hatua ya 1.

Utakuwa kwenye faragha wewe pamoja na mtoa huduma wako wa afya - kwa kawaida daktari, muuguzi, au mfanyakazi wa afya.




Hatua ya 2.

Utaambiwa kuvua nguo zako kutoka chini ya kiuno na kulala kwa mgongo (kulala chali). Utapewa shuka la kujifunikia.



Hatua ya 3.

Daktari au muuguzi atatumia kifaa kinachoitwa spekulum, kurahisisha kufikia mlango wako wa uzazi.




Hatua ya 4.

Daktari au muuguzi watachukua kipimo kidogo cha seli kutoka kwenye mlango wako wa uzazi kwa kutumia brashi laini. Unaweza ukahisi usumbufu kidogo lakini hupaswi kusikia maumivu. Ikiwa utasikia maumivu, basi mwambie mtoa huduma wako mara moja.



Hatua ya 5.

Mtoa huduma wako wa afya atatuma kipimo kile kwenye maabara ya ugonjwa ili kikapimwe.



Hatua ya 6.

Huko kwenye maabara kipimo chako kitapimwa kuona kama kina ugonjwa wa virusi vya HPV. Majibu ya kipimo hiki yatapelekwa kwa mtoa huduma wako.